



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

**Kumb.Na. MM/AR/S.20/12/106**

**24.05.2023**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha amepokea kibali cha kutekeleza Ikama na Bajeti kwa Ajira Mpya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 chenye Kumb.Na.FA.971/288/01/TEMP/06 cha tarehe 06 April, 2022 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Hivyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha anawatangazia wananchi wote ambao ni Raia wa Tanzania wenye sifa kuomba nafasi zilizoorodheshwa hapa chini: -

**DEREVA DARAJA LA II – NAFASI 2 - TGS B**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- Awe amefaulu kidato cha nne (iv) au cha sita (vi).
- Leseni ya daraja E au C ya Uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**MAJUKUMU YA KAZI YA UDEREVA:**

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi..
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali,
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya usafi wa gari na;
- Kufanya kazi nyingine kadri utakavyoelezwa na Msimamizi wa kazi.

**MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA III (NAFASI 2): - TGS C**

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

- Awe amefaulu kidato cha nne (IV)
- Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu ngazi ya Stashahada (Diploma) kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amefaulu somo la hati mkato ya Kiswahili na Kiingereza, maneno yasiyopungua 80 kwa dakika moja.
- Awe na cheti cha programu ya windows, Microsoft office, Internat-E-mail na Publisher, Power point kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali.

**KAZI NA MAJUKUMU MWANDISHI MWEENDESHA OFISI DARAJA III**

- Kuchapa barua taarifa na nyaraka za kawaida na SIRI.
- Kupokea wageni na kuwasaidia shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikia.
- Kutunza taarifa za kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wako na ratiba ya kazi nyingine.
- Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- Kupokea majalada na kusambaza kwa maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika.
- Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- Kupanga dondoo na kufanya maandalizi ya Vikao mbalimbali.
- Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi.

**MASHARTI YA UJUMLA:**


Mwombaji awe Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45

- Mwombaji aambatanishe nakala ya kadi ya NIDA
- Mwombaji aambatanishe cheti cha kuzaliwa
- Mwombaji aambatanishe maelezo yake binafsi (CV) pamoja na namba za simu zinazopatikana muda wote
- Mwombaji awe na wadhamini watatu na namba za simu ambazo zinazopatikana muda wote
- Mwombaji wakati wa kuwasilisha maombi aweke picha ndogo (Passport size) moja iliyoandikwa jina kwa nyuma na ibandikwe kwenye barua ya maombi.
- Barua ziandikwe kwa mkono na ziambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu pamoja na taaluma.
- Testimonial, Provisional result, statement of result **HAVIKUBALIKI**

- Waombaji wote ambao wamesoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimefanyiwa ulinganishi na TCU na NACTE na kuambatanisha taarifa kutoka Mamlaka husika.
- Madereva waambatanishe maombi la Leseni ya udereva.
- Waombaji wote watatakiwa kuangalia mara kwa mara kwenye tovuti wa Halmashauri kwa sababu watakoitwa kwenye usaili wa awali majina yao yatawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ambayo ni [www.arushadc.go.tz](http://www.arushadc.go.tz)
- Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 06.06.2023.
- Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili "HAYATAFIKIRIWA".

**MAOMBI YOTE YATUMWE KWA NJIA YA POSTA KATIKA ANUANI IFUATAYO:**

MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA,  
S.L.P 2330,  
ARUSHA.

  
Seleman H. Msumi

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA ARUSHA  
ARUSHA